

C. KUTAFAKARI NENO

Katika sala ya Jumuiya tunatafakari Neno la Mungu wala hatutoi mahubiri.

- Msomaji asome somo mara ya kwanza taratibu kisha kuwe na muda mfupi (**dakika 2 au 3 za tafakari**). Wote wasikilize kwa makini.
- Kisha msomaji au mtu mwingine alisome somo kwa mara ya pili.
- Kila mtu ataje neno au maneno yaliyomgusa kwa sauti bila kuongeza maneno mengine.
- Baada ya kila mtu kutaja neno liliomgusa msomaji asome somo kwa mara ya tatu.
- Kila mmoja apewe nafasi ya kushirikisha kwa nini neno au maneno aliyotaja yamemgusa bila kuhubiri. Aseme neno limemfundisha nini au linamhimiza kufanya nini.

D. SALA YA WAAMINI

Baada ya kila mmoja kushirikisha Neno inafuata sala ya waumini. Hii ni sala ya kuombea kanisa na mahitaji ya wanajumuiya.

E. SADAKA

Kila wanaposali wanajumuiya watoe sadaka. Sadaka hii iwekwe vizuri na kupelekwa ofisi ya Parokia kwa ajili

ya kuhifadhiwa.

F. SHUKRANI

Kila familia au muumini aliyeko ataje Mungu amembariki kwa njia zipi.

Sala ya kumshukuru Mungu kwa baraka na neema ndani ya boma.

Kila mmoja ataje mahitaji ya familia yake au yeyé binafsi.

Sala ya kuombea mahitaji.

Matendo ya huruma: Jumuiya iangalie mahitaji ya wanajumuiya wasiojiweza.

Jumuiya kwa pamoja au kila mmoja aseme atakayofanya ili kusaidia wasiojiweza.

Jumuiya iseme itawasaidiaje wasiojiweza.

Baada hayo. Sala ya ya mwisho. Tunaukimbia ulinzi wako mzazi mtakatifu wa Mungu

Sala ya jumuiya izunguke kila boma kila ijumaa



MWONGOZO WA JUMUIYA NDOGOGO



MAANA YA JUMUIYA

Maana ya jumuiya ndogondogo za Kikristu ni familia kadhaa za Kikristu wanaoishi pamoja, kusali pamoja na kuishi imani yao kwa pamoja. Kila mbatizwa anapaswa kushiriki katika sala ya Jumuiya (Mtd 2:42-47).

A. MWANZO

Wanajumuiya wote wakusanyike katika boma moja saa waliopanga bila kuchelewa. Mahali pa sala pawe pameandaliwa vizuri. Kuwe na msalaba, Biblia, mshumaa uwakao na shajara au misale ya waumini. Ikiwezena ni vema wanaboma wangoze sala ya Jumuiya inapokutana kwenye boma lao.

UTARATIBU WA SALA

Wimbo

- Kiongozi afungua kwa sala.
- Ibada ya toba (sala ya namuungamia na Bwana utuhurumie)
- Kila mmoja ajiangalie ni wapi amekosea Mungu na Jirani yake.
- Kila mmoja aombe msamaha kwa Mungu na kwa yule aliyemkosea

B. KUSOMA NENO

- Somo laweza kuwa la siku hiyo au la Jumapili iliyopita au ijayo.
- Msomaji asome vizuri na kwa sauti inayosikika na kila mtu. Ni vizuri atakayesoma somo alipitie kabla ili aweze kusoma vizuri.

Fr. Lawrence Muthee, SVD